# KEZILAHABI NA THOMAS HARDY: SARAFU KWA YA PILI?

P.M. Musau

Hapana shaka kuwa Euphrase Kezilahabi ni miongoni mwa waandishi maarufu wa Fasihi ya Kiswahili. Mwandishi huyu ameandika riwaya zisizopungua tano na diwani mbili za mashairi. Kazi hizi husomwa sana katika shule na vyuo vya Afrika ya Mashariki. Maandishi ya Kezilahabi pia yamejadiliwa kwenye majarida ya fasihi, tasnifu za shahada za juu, na kwenye makongamano mbali mbali yanayohusu fasihi ya Kiswahili.

Baadhi ya masuala yaliyokwisha kushughulikiwa na wahakiki wa kazi za Kezilahabi ni pamoja na msimamo unaoelekea kukatisha tamaa katika riwaya zake (Masau 1995) na ukengeushi wa wasomi katika kazi zake (Mayaka 1991), miongoni mwa masuala mengi mengineyo.

Ingawa tahakiki nyingi zimeandikwa kuhusiana na maandishi ya kifasihi ya Kezilahabi, hakuna mhakiki tunayemjua aliyeshughulikia ushabihiano uliopo kati ya riwaya yake ya kwanza iitwayo *Rosa Mistika* na kitabu cha Thomas Hardy, kinachoitwa *Tess of the D'Urbervilles* kilichoandikwa katikati ya karne ya kumi na tisa kule Uingereza.

Hilo ndilo suala litakaloshughulikiwa katika makala hii. Hata hivyo, ni vizuri kutahadharisha msomaji kuwa makala hii haina nia ya kuipima riwaya ya Kezilahabi kwa kutumia mizani ya riwaya ya Thomas Hardy ili kukadiria deni la Kezilahabi kwa mwandishi huyo. Hilo ni jambo lisilowezekana kwa sababu kila kazi ya fasihi huwa inajitosheleza yenyewe.

Riwaya ya *Rosa Mistika* ambayo ndiyo ya kwanza ya Kezilahabi ilichapishwa mwaka wa 1971. Riwaya hii iliyopigwa marufuku na wakuu wa chama tawala Tanzania ilipochapishwa kwa mara ya kwanza, ni hadithi ya msichana mzaliwa wa kijiji aitwaye Rosa Mistika. Hadithi hii inaonyesha sura mbali mbali za maisha ya mhusika huyu mkuu. Tulipokutana naye kwa mara ya kwanza, Rosa Mistika yuko kijijini chini ya ulinzi wa baba yake. Baadaye tunamwona katika shule ya Misheni inayosimamiwa na watawa wa kikatoliki. Halafu tunashuhudia vituko vya Rosa akiwa kwenye chuo cha ualimu na akiishi kwenye miji ya Tanzania ambapo anakumbana na ukatili wa maisha ya kisasa. Msichana huyo anashindwa kustahimili vishindo vya maisha ya kisasa kwa sababu hakulelewa vizuri kukabiliana na maisha ya aina hiyo. Ushinde huo unamfanya kukata tamaa na baadaye kujiua.

Riwaya ya *Tess of the D'Urbervilles* tutakayoilinganisha na *Rosa Mistika* ilichapishwa kama kitabu mwaka wa 1892. (Ni sadfa iliyoje kuwa kitabu hiki nacho kilikataliwa na wachapishaji hapo mwanzoni kwa sababu walikiona kuwa kitabu kisichoambatana na maadili ya jamii ya Uingereza ya wakati huo!). Hii ni hadithi ya msichana aitwaye Tess Durbeyfield. Hadithi hii inatuonyesha hatua tofautitofauti za maisha ya mhusika mkuu Tess. Familia yake inapofiwa na farasi wao waliyemtegemea sana, wazazi wa Tess wanamshauri kwenda kwa mwanamke mmoja wa familia yenye jina D'Urberville ili akatafute msaada huko. Huko anakoenda Tess anakutana na mwana wa kiume wa nyumba hiyo, Alec, ambaye anambaka. Matokeo ya kitendo hicho ni kwamba Tess anarudi kwao akiwa mja mzito. Anajifungua mtoto ambaye kwa sababu ya ugonjwa hajaliwi kuishi. Kifo cha mtoto huyo kinamwezesha Tess kwenda kutafuta kazi mahali pengine. Anapata kazi kwenye shamba la ufugaji wa ng'ombe. Huko anachumbiwa na kijana aitwaye Angel Clare. Kwa sababu zisizoeleweka Tess hakufanikiwa kumwelezea mchumba wake

mpya kuhusu maisha yake ya hapo awali. Ni baada ya arusi tu, Tess anapomwelezea Angel yale yaliyompata huko nyuma. Angel anaamua kumuacha Tess na kuhamia Brazili. Baadaye Tess anakutana na mbaya wake wa zamani, Alec, na kufanya urafiki naye. Baadaye kidogo Angel anarejea kutoka Brazil akiwa na majuto mengi kuhusu kitendo alichomtendea Tess. Baada ya kurejea kwa Angel, Tess anapandwa na hasira na kumuua alec. Anaungana tena na Angel! Muungano huo haudumu kwa sababu baada ya muda si muda Tess anatiwa mbaroni na polisi na kunyongwa kwa sababu ya kumuua Alec.

Ingawa riwaya hizi mbili ziliandikwa katika nyakati tofauti katika tamaduni zisizofanana, inamdhihirikia anayezisoma kwa makini kuwa zina mambo mengi yenye kufanana. Mwanzo kabisa, hadithi zote mbili zinahusu wasichana washamba ambao ni limbukeni wa maisha. Wahusika hawa wakuu wana umri unaokaribiana sana (mmoja ana miaka kumi na mitano ilhali yule mwingine ana kumi na sita). Isitoshe, wahusika wote wakuu wamezaliwa kwenye familia za watoto sita (mtoto wa sita kwenye riwaya ya Kezilahabi yumo tumboni mwa mamake). Mbali na hayo, wahusika hawa ni mabinti za wazazi wasiojali sana namna wanavyoendesha maisha yao na familia zao. Kwa mfano, baba yake Rosa, Zakaria, ni mlevi wa kupindukia ambaye ameshindwa kabisa kuikimu familia yake. Mwandishi anatupa habari ifuatayo kumhusu Zakaria:

> Zakaria alikuwa mwalimu zamani, lakini alifutwa kazi kwa sababu ya ulevi. Jirani zake walisema alijali pombe kuliko watoto: alikuwa hajatoa hata chapa kuwalipia ada ya shule. .... sasa watoto walikuwa shuleni, heko kwa mama yao (uk.11).

Maelezo haya yanaelezea pia tabia ya baba yake Tess. Tabia ya mzee huyo inawachukiza sana watoto wake. Kwa mfano, wakati mmoja Tess anasema maneno haya baada ya kuchukizwa na ulevi na tabia ya baba yake:

> Alifanya hivyo kwa nini?
> Nilitamani kuzama ardhini kwa
> haya (uk.12 - tafsiri yetu).

Pamoja na ulevi, wazazi wa wahusika hawa wakuu wa riwaya tunazozungumzia wamelewa kasumba fulani. Tunachomaanisha hapa ni kwamba, wazazi hawa wanashikilia imani fulani ambazo hawataki kuziacha. Kasumba hizi zinawaletea madhara makubwa watoto wao. Kwa mfano, Rosa Mistika analelewa na baba anayeamini kuwa mabinti huchungwa kama mahabusu ili wasitangamane na wavulana. Mzee huyo huamini kuwa binti zake wapaswa kutenganishwa kabisa na watoto wa kiume. Anaamini kuwa hayo ni malezi bora ambayo ufanisi wake utaonekana pale mabinti hao watakapomletea mahari baada ya kuolewa. Ama malezi ya aina hiyo yanapelekea Rosa kutofahamu namna ya kukabiliana na matatizo yanayotokana na maisha ya kisasa nje ya kijiji chao na mbali na jicho kali la baba yake. Matokeo ya kasumba hii ya malezi ni kwamba, Rosa anaponzwa na maisha. Kuponzeka huko kunadhihirika pale anapojiua.

Wazazi wa Tess kwenye Riwaya ya Thomas Hardy nao wanaongozwa na kasumba ya kujivunia 'ukoo wao'. Mtu fulani amewadanganya kuwa baba yake Tess ana uhusiano wa damu na familia moja yenye kusifika kwa utajiri wake. Baba yake Tess anaziamini habari hizo bila ya kuzichunguza. Habari hizo zinamlewesha. Kwa sababu ya kuamini habari zisizo za kweli, anamtuma binti yake mbali na kwao kwenda kutafuta usaidizi. Huko Tess anakutana na muhuni anayempachika mimba na kumharibia maisha yake. Baadaye binti huyo anamuua muhuni huyo na kusababisha kifo chake mwenyewe.

Sio wazazi wa wahusika wakuu tu walio na imani wasizotaka kuzibadilisha. Wachumba wa wahusika hawa wakuu wana kasumba yao:

hawa wangetaka kuoa mabikira. Kwa mfano, Angel katika kitabu cha Hardy angependa kuoa bikira ingawa hakuna ushahidi wowote kwenye riwaya unaotuonyesha kuwa Angel mwenyewe ni bikira. Vile vile, Charles katika riwaya ya Kezilahabi naye anatamani sana kuoa bikira ingawa ubikira wake ni jambo la kutiliwa shaka.

Uwiano zaidi unapatikana kati ya riwaya tunazozichambua tunapochunguza maudhui muhimu yanayojitokeza katika riwaya hizo. Kulingana na maoni ya Rutland (1962:229), maudhui muhimu katika *Tess of the D'Urbervilles* yanahusu adhabu wanayopewa wasiokuwa na hatia badala ya wale wenye lawama. Hebu na tutafute ushahidi wa kauli hii kwenye riwaya zote mbili.

Katika riwaya ya Hardy kuna matukio kadha yanayotudhihirishia kwamba wale wasiokuwa na hatia huadhibiwa badala ya wale wenye hatia. Jambo hili linadhihirika tunaporejelea kwa ufupi baadhi ya matukio muhimu ya mhusika mkuu Tess. Kwa mfano, farasi wa familia yao anapokufa, wazazi wa Tess wanamshauri kwenda kwa mwanamke mmoja kutafuta usaidizi. Huko anakoenda ndiko anakokutana na muhuni anayembaka. Matokeo ni mimba na baadaye kuzaliwa kwa mtoto. Anapozaliwa mtoto, Tess analazimika kumbatiza mtoto wake mwenyewe kabla hajafa (mtoto) kwa sababu kasisi hayuko radhi kumbatiza mtoto haramu ambaye ni zao la dhambi ya mwanamke. Isitoshe, baada ya kifo cha mtoto huyo, wakuu wa dini wanakataa kumzika kwenye ardhi takatifu wanakozikwa wakristo. Pamoja na hayo, itakumbukwa pia kwamba Tess ameachwa na mchumba wake wa pili kwa sababu si bikira. Matukio haya na mengine mengi, yanaelekea kutuonyesha kwamba katika dunia iliyojaa unafiki wa kila aina wasio na lawama huadhibiwa badala ya wale wenye kutenda maovu.

Maudhui yanayojitokeza katika riwaya ya Kezilahabi, miongoni mwa mengine, ni yayo hayo. Jambo hilo linadhihirika tunapoyafuatilia maisha ya Rosa Mistika aliye mhusika mkuu kwenye riwaya ya Kezilahabi. Kwanza, Rosa amelelewa na baba mkali. Baba huyo ana kasoro mbili, ni mlevi, na pili, ni mtu anayetaka kumlea binti yake kwa kuzingatia mila za zamani zilizopitwa na wakati. Pia, Rosa anapelekwa katika shule ya misheni ambayo haimuandai kukabiliana na maisha. Ama malezi ya aina hiyo hayamuandai Rosa kukabiliana na maisha ya kisasa. Anaangukia mitego mbalimbali kwa sababu ya uanagenzi wake. Kwa mfano, anakubali kufanya urafiki na 'shuga dadi' kwa sababu ya kukosa uzoefu wa kimapenzi. 'Shuga dadi' huyo anaelezwa ifuatavyo na mwandishi:

> Deogratias alikuwa mmoja kati ya wale wazee wanaojifikiria bado ni vijana. Wazee wanaopendelea kutembea na vitoto vidogo - hata vile vinavyoanza kutoa maziwa. Watoto wao wa kuzaa. Wazee wasioona aibu... Akiwa na umri wa miaka arobaini na miwili, alikuwa bado akiwaandikia wasichana barua akisema ninakupenda kama almasi ya Mwadui (uk.50).

Katika riwaya hii ya Kezilahabi, tunaweza kusema kuwa wale waliochangia kuharibika kwa tabia ya Rosa na hatimaye kuangamia kwake ni wale waliomlea, waliomsomesha na wale waliokuwa na mamlaka katika jamii. Hata hivyo, wale waliomlea wawe ni wazazi wake, waalimu wake au watu walio na mamlaka katika jamii - wazee akina Deogratias - hawaadhibiwi, badala yake Rosa mwenyewe ndiye anayehangaishwa na baadaye kulipia yale yaliyompata kwa kuhukumiwa kifo. Mashaka yanayompata Rosa yanatudhihirishia kuwa wasio na hatia aghalabu huadhibiwa badala ya wale walio nayo.

Ulinganifu zaidi unaopatikana katika riwaya mbili tunazozichambua unahusu misingi ya majaaliwa iliyotumiwa na waandishi wa riwaya zote mbili kuendeleza hadiithi zao. Ni wazi kuwa wahusika wakuu katika kazi hizi mbili wamejaaliwa bila hiari yao kuangamia. Kuna mifano kadha kwenye riwaya hizi inayothibitisha madai hayo. Tuchukue, kwa mfano, maumbile ya wahusika wakuu. Wote wanavutia sana kimaumbile katika tamaduni zao. Mathalan, Tess wa Hardy ana 'mdomo mwekundu unaofanana na ua', 'uso uliorembeka', na 'umbo linalopendeza'.

Naye Rosa wa Kezilahabi ni 'msichana anayependeza', 'mwenye kimo cha wastani', 'mpole na mnyamavu'. Maumbile ya wahusika hawa ni chanzo cha matatizo wanayoyapata katika maisha yao. Hawana njia ya kubadilisha maumbile yao ili wasipendwe na wengi. Maumbile, jambo wasilokuwa na hiari nalo, ndiyo yanayowaletea maangamizi.

Kuna matukio kadhaa kwenye riwaya hizi yanayozidi kututhibitishia kwamba wahusika wakuu wamejaaliwa kupatwa na yale yaliyowapata. Matukio hayo yanatufanya tuhisi kuwa wahusika hao wamenaswa mtegoni na kwamba hawawezi kujinasua. Aidha matukio hayo yanatubainishia kuwa wahusika hao hawawezi kutumia uwezo wao wa kibinadamu kuyabadilisha yale yaliyokwishaandikwa. Sio Tess wa Hardy wala Rosa wa Kezilahabi anayeyadhibiti maisha yake. Maisha yao yanaendeshwa tu. Katika riwaya hizo hatuoni mhusika akitenda jambo linaloweza kuboresha maisha yake. Tuchukue mfano wa Rosa kwenye riwaya ya Kezilahabi. Msichana huyu analelewa vibaya na baba yake; shule nayo haimsaidii kuyaelewa masuala ya kidunia; baadaye anayumbishwa na maisha na hatimaye kujiua. Huu si mfano wa mtu anayeyadhibiti maisha yake. Maisha ya mhusika huyu yanaendeshwa na nguvu fulani zilizo nje ya uwezo wake.

Maisha ya Tess wa Hardy yanaweza pia kuelezewa vivyo hivyo. Maisha hayo yanafululiza kwa namna inayoonyesha kuwa kuna nguvu fulani zinazoyaendesha bila ya hiari ya mhusika mwenyewe. Kuthibitisha jambo hilo Hardy anatumia maneno kama: "aliyejaaliwa", "aliyelaaniwa". Pamoja na matumizi ya maneno hayo, hadithi inapokaribia mwisho wake, na inapodhihirika kuwa Tess atanyongwa, mwandishi anasema kuwa miungu walikuwa wameuhitimisha mchezo wao na Tess. Haya yote yanatuelekeza kufikiria kuwa maisha ya Tess hayakuwa mikononi mwake lakini yalikuwa yanadhibitiwa au yanachezewa na miungu au viumbe wengine wenye nguvu za miungu.

Kimtindo, riwaya mbili tunazozizungumzia zina mengi yaliyofanana. Kwa mfano, kuna matumizi ya taswira kujenga dhamira ya mwandishi. Taswira hizo zinatumiwa kubashiria matukio muhimu. Kwa mfano, katika *Tess of the D'Urbervilles* watoto wanalia anapoondoka Tess nyumbani kwao kwa mara ya kwanza kwenda kwa familia ya D'Urberville; kulia huku ni ndege mbaya inayoashiria uovu atakaotendewa Tess anakoenda. Kadhalika, kabla ya Tess kufanyiwa unyama, mwandishi anatwambia kuwa yeye na mbaya wake hawangeweza kuiona njia vizuri kwa sababu kulikuwa na ukungu mwingi. Na kabla ya arusi ya Tess na Angel, mwandishi anaarifu kuwa jogoo aliwika; hii ni ishara inayotukumbusha kusalitiwa kwa Yesu. Taswira zote hizo tulizozitaja zinatufanya tutarajie matukio fulani mabaya.

Taswira za aina hiyo pia zinapatikana katika riwaya ya Rosa Mistika. Anapotubashiria yale yatakayompata limbukeni Rosa pamoja na dada zake, mwandishi anatupa taswira ya mwewe anayenyakua vifaranga wa kuku:

> Mwewe alikuwa amechukua kifaranga kingine zamu hii hakwenda mbali. Alitua juu ya mti karibu na mji. Wasichana walianza kumtupia mawe lakini hayakumfikia. Mwewe alikula kifaranga bila kujali. Alipomaliza aliruka kwa raha ya shibe... (ukl..22).

Mfano huu unatubashiria yale yatakayompata Rosa atakapoenda mbali na kijiji chao. Nayo hatari itakayomkabili Rosa akiwa kwenye shule ya Rosary inaelezwa hivi:-

> Rosa alikwenda shule ya Rosary... kulikuwa na milima karibu kila upande. Milima hii ilikuwa imejaa mawe makubwa meusi na mapango ambamo fisi walikuwa wakilala hapo (sic). Usiku utawasikia wakicheka lakini mchana hawaonekani (uk.28).

Kutokana na mifano ya matumizi ya taswira za aina hii, ni dhahiri kuwa Hardy na Kezilahabi wanatumia ishara kuyaendeleza maudhui katika riwaya zao. Kwenye riwaya hizo, mazingira wanamojikuta wahusika yanaonyesha uhusiano fulani na matukio yanayompata mhusika. Matumizi haya ya taswira yana dhima kubwa katika uendelezaji wa dhamira za waandishi tunaowachambua.

Riwaya tunazochambua zina hadithi zinazosikitisha sana kwa sababu ya yale yanayowapata wahusika wake wakuu. Ingawa hivyo, riwaya zote mbili haziwezi kuitwa tanzia (tragedy) kwa sababu hazitimizi vigezo vyote vya kinadharia kuziwezesha kupewa jina hilo. Kigezo kimoja kikuu katika tanzia ni kuwa mhusika hung'ang'ania kulifanya jambo na kupuuza ushauri anaopewa na watu wengine. Hayo anayasisitiza Kramer (1991:74) anapotuarifu kuwa:

> Kigezo kimoja kikubwa cha tanzia, na kinachopatikana katika maelezo, ni ile hali ya kung'ang'ania kufanya jambo - kwa mfano, mhusika kung'ang'ania kufanya lolote ili kutimiza lengo lake pasina kujali maoni ya wengine... (tafsiri yetu).

Hivyo sivyo walivyo wahusika katika riwaya tunazohakiki. Tumeona kuwa wahusika wetu hawana udhibiti wa matendo yao. Hii ni kwa sababu maisha yao yanaendeshwa na nguvu zisizoonekana. Wao wenyewe hawana hiari ya kufanya jambo. Kwa sababu hiyo, tunaweza kusema kuwa kigezo cha kung'ang'ania kufanya jambo ambacho ni muhimu katika tanzia hakipo katika riwaya zote mbili.

Katika makala hii tumejadili uwiano uliopo kimaudhui na kimtindo kati ya riwaya mbili zilizoandikwa katika nyakati tofautitofauti za kihistoria na katika tamaduni zinazotofautiana. Jambo linalotushangaza sio kwamba mwandishi mmoja huenda aliathiriwa na mwingine. Linalotushangaza hasa ni kuwa hadithi mbili zilizobuniwa kwa kutumia mali ghafi kutokana na jamii tofautitofauti zina uwiano mkubwa jinsi hiyo.

## Marejeo


Hardy, T. (1991): *Tess of D'Urbervilles: An Authoritative Text Background and Sources criticism.* Toleo la Tatu, Mhariri: Elledge, W.W. Norton and Company, New York.

Kezilahabi, E. (1980): *Rosa Mistika.* Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Kramer, D. (1991): *Thomas Hardy: Tess of the D'Urbervilles.* Cambridge: University Press, Cambridge.

Lindley, D. (1986): *Notes on Tess on the d'Urbervilles: Thomas Hardy.* Longman, York Press.

Mayaka, G. (1991): *Ukengeushi wa wasomi katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi.* Unpublished M.A. Dissertation Kenyatta University.

Musau, P.M. (1985): *E. Kezilahabi: Mwandishi Aliyekata Tamaa.* Unpublished M.A. Dissertation, University of Nairobi.

Rutland, R.w. (1962): *Thomas Hardy: A Study of his Writings and their Background.* Russell and Russel Inc. New York.

Waldhoff, L. (1075): 'Psychological Determination in *Tess of the D'Urbervilles*'. Katika: *Critical Approaches to the Fiction of Thomas Hardy*. Edited by Kramer, D. Macmillan, London.